HALMASHAURI YA MJI HANDENI

16/05/2018

TANGAZO LA ZABUNI

Halmashauri ya Mji wa Handeni inawatangazia wafanyabiashara/makampuni/ushirika/vikundi kuwa inahitaji kupata wazabuni wenye uwezo wa kukusanya mapato/huduma ya Ulinzi kwa niaba ya Halmashauri kuanzia tarehe 01/07/2018 hadi tarehe 30 Juni 2019 kwa mujibu wa sheria ndogo za Halmashauri kama ilivyoainishwa hapo chini-

ZABUNI ZA USHURU/HUDUMA YA ULINZI

NAMBA YA ZABUNI	JINA LA ZABUNI
LGA/172/2018/2019/NC/01	Ushuru wa Mazao ya Misitu, Madini ya Ujenzi (mchanga, kokoto, mawe, tofali na kifusi).
LGA/172/2018/2019/NC/02	Ushuru wa Mazao ya Kilimo
LGA/172/2018/2019NC/03	Ushuru wa Mnada Nderema, Machinjio, Soko la kuku Chogo (Zizini) na Ushuru wa Magulio Msaje na Mabanda
LGA/172/2018/2019/NC/04	Huduma ya Ulinzi na Mali za Halmashauri

MASHARTI YA ZABUNI

1. Mwombaji asiwe anadaiwa na Halmashauri ya Mji wa Handeni
2. Mwombaji anatakiwa kulipa ada ya zabuni ni**Tshs. 100,000/=** ambayo haitarudishwa.
3. Mwombaji atatakiwa kufanya utafiti wa kina katika chanzo husika ili kuepuka migogoro katika ulipaji wa mapato.
4. Mwombaji awe na uzoefu wa kukusanya mapato usiopungua miaka 2
5. Mzabuni atatakiwa kuingiza makusanyo ya kila siku kwenye akaunti ya Mapato ya Ndani ya Halmashauri ya Mji wa Handeni.
6. Mwombaji awe tayari kutumia mashine za kieletroniki zitakazotolewa na Halmashauri kwa vituo vyote vya kukusanyia Mapato.
7. Mzabuni aeleze ni kiasi gani ataweza kukusanya kwa Mwezi na asilimia ngapi atapewa kama gawio la kazi ya Uwakala. Vile vile Mzabuni awe tayari kuweka asilimia 75 ya kiasi alichokieleza kuwa atakikusanya kwa Mwezi ili kiwe dhamana yake.
8. Mwombaji awe na leseni hai ya biashara husika, iwe na usajili wa kuandikishwa kampuni, TIN, aeleze Ofisi yake ilipo (Physical Location) na aambatanishe taarifa za benki (bank statement) ya Miezi Sita iliyopita tokea tarehe ya Tangazo hili pamoja na Power of Attorney kwa Makampuni
9. Vitabu vya Zabuni na maelekezo mengine vinapatikana ofisi ya Katibu wa Bodi ya Zabuni, S.L.P.51, Handeni, kuanzia saa 2.30 asubuhi mpaka saa 9.30 alasiri (Jumatatu-Ijumaa).

10. Nyaraka za maombi ziwe tatu (**halisi moja na nakala mbili)** iliyofungwa kwa LAKIRI, iandikwe juu ya bahasha **"NAMBA NA JINA LA ZABUNI INAYOOMBWA"** na zitumbukizwe katika sanduku la zabuni lililoko Makao Makuu ya Halmashauri ya Mji wa Handeni. Zitumwe kwa anwani ifuatayo:-

KATIBU
BODI YA ZABUNI HALMASHAURI YA MJI
S.L.P.51, HANDENI

11. Mwisho wa kupokea zabuni ni tarehe 29/05/2018 saa 05:00 Asubuhi. Zabuni zitafunguliwa muda huo huo katika ukumbi wa mikutano Makao Makuu ya Halmashauri ya Mji Handeni na waombaji mnakaribishwa katika ufunguzi kwa gharama zenu.
12. Mwombaji awe na vitendea kazi vya kutosha kumudu vyema Zabuni aliyoomba
13. Mzabuni atawajibika kukusanya mapato ya Halmashauri pamoja na kumchukulia hatua yeyote ambaye atakwamisha zoezi la ukusanyaji mapato kwa mujibu wa sheria za fedha za Serikali za Mitaa za Mwaka 1982, pamoja na sheria ndogo za Halmashauri ya Mji.
14. Kwa waombaji wa kutoa Huduma ya Ulinzi na Mali za Halmashauri, masharti ya Zabuni yanapatikana kwenye kabrasha la Zabuni.

KARIBU SANA HANDENI, TUFANYE KAZI

KENNETH K.HAULE
MKURUGENZI
HALMASHAURI YA MJI
HANDENI